# Kiswahili Quiz - 7

**Jibu maswali yafuatayo kisha bonyeza "Mark Now" kuona majibu.**

**QUESTION 1**

Taja ngeli zilizotumika katika tungo hizi

a) Askari aliyekamata mwizi amefukuzwa kazi

b) Kucheka kwangu kusitafsirwe vibaya

c) Kitanda cha mototo kimenunuliwa posta

d) Kule kijijini kuna wageni wengi wasiojua Kiswahili

e) Shati lake limechanika vibaya

**QUESTION 2**

Onyesha upatanish wa kisarufi uliopo ni kati ya aina ya maneno

a) Mawe yameporomoka leo asubuhi

b) Hiki ndicho nilichokipata

c) Babu huyu anayezungumza sasa ni jirani yetu kabisa

d) Chausiku ni mwanaye

e) Mimi naitwa Kizito

**QUESTION 3**

Bainisha virai Nomino vilivyotumika katika tungo hizo

a) Gari letu lilileta matatizo njiani

b) Khamisi atamwona Mussa kesho

c) Mjomba aliyetaka kutudhurumu mali yetu amefungwa

d) Mji wa Arusha  ni mdogo sana

e) Someni kwa bidii

**QUESTION 4**

Tunga sentensi kuonesha

a) Kirai kielezi

b) Kirai kivumishi

c) Kirai nomino

d) Kirai kitenzi

e) Kirai kiunganishi

**QUESTION 5**

Bainisha vishazi tegemezi vilivyopo katika tungo hizi

a) Somo lililoongezwa kwenye cheti ni batili

b) Kijana unayemwona hivisasa ndiye kaka yangu

c) Anacheka anavyolia kwa sauti kubwa

d) Siku zote ninapenda mtu anayesema ukweli

e) Tulivyomuuliza tu, alikimbia mbio.

**QUESTION 6**

Eleza kwa kutoa mifano miwili kati ya

a) Sentensi sahili

b) Sentensi shurutia

c) Sentensi changamano

d) Sentensi ambatano

**QUESTION 7**

Katika sentensi zifuatazo bainisha kiima na kiarifu

a) Anayesoma darasa la kwanza anaimba jukwaani

b) Siku usiyoijua utamwona akirudi

c) Watu wote waliomsikiliza mzee Yule wamedanganywa

d) Leo mtihani huu nitafaulu kabisa

e) Sijawahi kumuona kuku akinywa soda

f) Juma ni rafiki yangu.